# RESEARCHERS, ACADEMICIANS AND ALLIED WORKERS UNION

# (RAAWU)

## *MWONGOZO WA UCHAGUZI*

**Toleo la 2021**

# CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU, SAYANSI, TEKNOLOJIA, UFUNDI STADI, HABARI NA UTAFITI

## (R A A W U)

## MWONGOZO WA UCHAGUZI

### 1.0 UTANGULIZI

1.1 Mambo ya msingi yanayohusu uchaguzi yamewekwa bayana kwenye Katiba ya RAAWU ya mwaka 2005 na kama yalivyorekebishwa mwaka 2009 na Kanuni zake toleo la 2005. Nia ya Mwongozo huu ni kusadia wanachama, Viongozi na watendaji wa Chama katika kutekeleza yale yaliyomo ndani ya Katiba na Kanuni zake toleo la 2005.

1.2 Ni wajibu wa kila mwanachama, viongozi na watendaji wa Chama, wagombea, wapiga kura na wasimamizi wa uchaguzi, kuuelewa vizuri Mwongozo huu na kuheshimu yaliyomo ndani yake.

1.3 Mwongozo huu utasomwa pamoja na Katiba ya RAAWU ya mwaka 2005 na Kanuni zake toleo la mwaka 2005.

1.4 Watendaji Wakuu wa Ofisi za Kanda na Makao Makuu watakuwa na wajibu wa kutoa ufafanuzi na tafsiri kuhusu yaliyomo kwenye mwongozo huu pale itakapojitokeza haja ya kufanya hivyo.

### 2.0 MAANDALIZI YA WANACHAMA (WAPIGA KURA) KABLA YA UCHAGUZI

2.1 Sekretarieti ya uchaguzi ya Kanda/Taifa ndio yenye jukumu la kuandaa na kuratibu shughuli zote za uchaguzi katika Kanda/Taifa.

2.2 Zoezi la uchaguzi litaambatana na utoaji wa elimu kwa Wanachama, kabla ya kupiga kura.

2.3 Elimu hiyo ilenge katika kuwafahamisha wanachama juu ya mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi nchini yanayotokana na msukumo wa utandawazi na athari zake katika soko la kazi.

2.4 Elimu hiyo iweke bayana changamoto zilizopo kwa RAAWU katika kukabiliana na mabadiliko yanayoelezwa hapo juu, ikiwa ni pamoja na utendaji wa RAAWU katika mazingira yenye Vyama vya Wafanyakazi zaidi ya kimoja katika Taasisi au Sekta moja.

2.5 Ni jukumu la kiongozi wa Kanda husika kwa kushirikiana na uongozi wa RAAWU Taifa kuandaa na kuratibu utoaji wa elimu hiyo.

2.6 Chaguzi katika Kanda zitaanza rasmi mwezi April hadi Septemba ya kila mwaka wa uchaguzi na uchaguzi Mkuu wa Taifa utafanyika kama itakavyoamuliwa na Baraza Kuu la Taifa.

## 3.0 HAKI YA KUCHAGUA NA KUCHAGULIWA

3.1 Mwanachama yeyote aliyetimiza wajibu na masharti ya uanachama kama yalivyobainishwa kwenye Katiba ya RAAWU atakuwa na haki ya kushiriki shughuli zote za uchaguzi ikiwa ni pamoja na kuchagua au kuchaguliwa.

3.2 Hakutakuwepo na vitendo vyovyote vile vya ubaguzi kwa msingi wa dini, kabila, jinsia, eneo, sura au ulemavu.

3.3 Mwanachama anayetaka kugombea nafasi yoyote ile atawasilisha jina lake kamili kwa Sekretarieti ya Kanda/Taifa akionyesha nafasi anayotaka kugombea, mahali pake pa kazi, anuani na wasifu wake. Mwanachama anaweza kugombea nafasi zaidi ya moja.

3.4 Kamati ya usimamizi ya uchaguzi itahakikisha kuwa wasifu wa kila mgombea unawekwa bayana kwa wapiga kura.

3.5 (i) Mkutano Mkuu wa Kanda utawachagua viongozi na wajumbe kama ilivyoainishwa kwenye Katiba ya RAAWU ya mwaka 2005 na kama ilivyorekebishwa mwaka 2009 kifungu 6.3(A)3.

(ii) Mkutano Mkuu wa RAAWU Taifa utawachagua viongozi na wajumbe kama ilivyoainishwa kwenye Katiba ya RAAWU ya mwaka 2005 na kama ilivyorekebishwa mwaka 2009 kifungu cha 7.5.

3.6 Mwanachama wa RAAWU ambaye ni kiongozi wa Chama cha siasa atakosa haki ya kuchaguliwa kuwa kiongozi wa RAAWU lakini atakuwa na haki ya kupiga kura. Hii ni kama inavyosisitizwa na Katiba ya RAAWU ya mwaka 2005 na kama ilivyorekebishwa mwaka 2009 kifungu cha 15.8 (a) na (b).

***"Tafsiri ya kiongozi wa chama cha siasa itaambatanishwa na mwongozo huu"***

## 4.0 KAMATI YA USIMAMIZI WA UCHAGUZI

4.1 Kutakuwepo na Kamati ya Usimamizi wa Uchaguzi.

Kamati hii itathibitishwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kanda/Taifa na muundo wake utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Afisa Kazi wa Mkoa unapofanyika uchaguzi, Afisa Kazi kutoka Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

(ii) Katibu wa RAAWU wa Kanda (uchaguzi wa Kanda). Au Katibu Mkuu au Mwakilishi wake (Uchaguzi wa Taifa).

(iii) Wajumbe watatu (3) watakaochaguliwa miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa (uchaguzi wa Taifa).

(iv) Wajumbe watatu (3) watakaochaguliwa miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kanda (uchaguzi wa Kanda).

4.2 Sekretarieti za Kanda na Taifa zitawezesha Kamati ya usimamizi wa uchaguzi kutekeleza majukumu yake, kwa kuandaa vifaa vyote muhimu vinavyohusika na uchaguzi na kuandaa mahali pa kufanyia shughuli zake.

4.3 Wajumbe wa kuchaguliwa watakaosimamia uchaguzi ni lazima wawe wamethibitisha kwamba hawatagombea nafasi yoyote ya uongozi.

**4.4 Kazi za Kamati ya Uchaguzi**

4.4.1. Kuandaa orodha ya majina ya wagombea kulingana na nafasi zinazogombewa.

4.4.2. Kuhakikisha kuwa ni wanachama hai tu ndio wanaoruhusiwa katika vikao vya Mikutano Mikuu ya uchaguzi.

4.4.3. Kupokea fomu za wagombea kwa lengo la kuzihakiki na kuhakikisha wanachama watakaotimiza masharti yaliyoko katika Kanuni za Katiba ya RAAWU toleo la 2005 kifungu cha 18.0 ndio watakaopitishwa kugombea nafasi za uongozi.

4.4.4. Kuhakikisha kuwa vifaa, ukumbi na mahitaji yote muhimu katika uchaguzi yamekamilika.

4.4.5. Kuhakikisha kuwa matangazo na taarifa ya mkutano inawafikia wajumbe na wagombea katika kipindi cha miezi miwili (2) (chaguzi za Kanda na kipindi cha miezi mitano (5) (chaguzi za Taifa).

4.4.6. Kuhakikisha kuwa taratibu za uchaguzi hazikiukwi kwa hali yoyote ile.

## 5.0 MAJINA YA WAGOMBEA

5.1 Sektetarieti za Kanda na Taifa zitaratibu majina yote ya wagombea kama yatakavyokuwa yanawasilishwa kwa kuandaa taarifa inayoonyesha jina, mahali pake pa kazi, nafasi anayogombea na wasifu wake.

5.2 Hata wale watakaoonekana kuwa hawana sifa za kugombea kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama, sharti majina yawasilishwe mbele ya Mkutano Mkuu na sababu za kutoruhusiwa kwao kugombea zielezwe bayana.

## 6.0 SIFA ZA MGOMBEA

Sifa za mgombea ni kama zilivyobainishwa katika Kanuni za Katiba ya RAAWU toleo la 2005 kifungu cha 18.0 – 18.1(i) – (vii).

## 7.0 MKUTANO WA UCHAGUZI

7.1 Mkutano wa uchaguzi utamchagua Mwenyekiti wa muda wa mkutano huo ambaye atatokana na wajumbe wa mkutano wa uchaguzi baada ya yeye mwenyewe kuthibitisha kuwa hatagombea nafasi yoyote ya uongozi.

7.2 Mwenyekiti wa Mkutano wa uchaguzi ataongoza mkutano kwa haki na usawa na atasaidiana na Kamati ya Usimamizi wa uchaguzi kuhakikisha kuwa Katiba na Kanuni za uchaguzi hazikiukwi.

## 8.0 UTARATIBU WA UCHAGUZI NDANI YA UKUMBI WA MKUTANO

8.1 Ni jukumu la Kamati ya Usimamizi ya uchaguzi kuthibitisha idadi ya wapiga kura.

8.2 Kabla ya zoezi la kupiga kura kila nafasi kuanza, wagombea watapewa fursa ya kujieleza mbele ya wajumbe kwa lengo la kuomba kura zao katika muda usiozidi dakika tatu na wanaweza kuulizwa maswali yasiyozidi matatu kwa kila mgombea.

8.3 Vitendo vyovyote vya ushabiki na ushangiliaji kwa waombaji wa kura havitaruhusiwa.

8.4 Upigaji kura utakuwa ni wa siri na si ruhusa kwa mtu yeyote kuuliza au kutazamia kile alichoaandika mpiga kura mwenzake.

8.5 Kila mjumbe atagawiwa karatasi maalum atakayoandika jina la mgombea ambaye ni chaguo lake.

8.6 Baada ya upigaji kura, kila mgombea atapewa fursa ya kuchagua mwakilishi wake kwenye zoezi la kuhesabu kura.

8.7 Kila karatasi ya kura itaangaliwa na kuhesabiwa.

8.8 Karatasi ya kura ambayo haikuandikwa chochote, jina au alama tofauti na maelekezo ya wasimamizi au ina majina ambayo hayapo kwenye orodha ya wagombea, kura hiyo itahesabiwa imeharibika.

8.9 Mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi atatangaza matokeo ya uchaguzi kwa utaratibu utakaokuwa umekubalika na Kamati.

8.9.1 Katika uchaguzi wa Kanda, ili Mwenyekiti atangazwe kuwa ni mshindi lazima apate zaidi ya nusu ya kura zote zilizopigwa.

8.9.2 Katika Katika uchaguzi wa Taifa, Mwenyekiti na Katibu Mkuu, ili watangazwe kuwa ni washindi ni lazima wapate zaidi ya nusu ya kura zote zilizopigwa.

8.9.3 Katika kura za makundi, washindi watapatikana kulingana na kuzidiana kwa wingi wa kura. Endapo kura zitalingana na mshindi/washindi hawajapatikana uchaguzi utarudiwa kwa wale tu wenye kura za juu.

8.9.4 Baada ya zoezi la kuhesabu kura kukamilika, karatasi zote za kura zitarudishwa kwenye masanduku ya kura na kuhifadhiwa vizuri kwa muda wa miezi sita.

## 9.0 NYONGEZA

9.1 Baadhi tu ya sifa za kiongozi wa RAAWU zimeainishwa na kuambatanishwa na mwongozo huu kama kielelezo cha kusaidia wanachama kupata kiongozi bora.

## 10.0 HITIMISHO

Mwongozo huu umetilia mkazo vipengele muhimu vinavyohusiana na uchaguzi kama vilivyoainishwa kwenye Katiba ya RAAWU toleo la mwaka 2005 na kama ilivyorekebishwa mwaka 2009.

Aidha, mwongozo huu umezingatia taratibu nyingine za kawaida zilizoonekana zinafaa na kukubalika kwenye mazingira ya uchaguzi ulio huru na wa haki.

***Mwongozo huu umeandaliwa na Kamati ya Utendaji ya RAAWU Taifa kwa idhini ya Baraza Kuu, mwaka 2016.***

.....................